easytvet.com

**1410/206**
**KISWAHILI**
**Oct./Nov. 2018**
**Muda: saa 3**

**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

**NATIONAL CERTIFICATE IN SOCIAL WORK DEVELOPMENT**

KISWAHILI

**Muda: saa 3**

**MAAGIZO**

*Mtihani huu una sehemu* ***NNE*** *muhimu:* ***insha, ufahamu, matumizi ya lugha na mbinu na vifaa vya kufundisha.***
*Jibu maswali yote kwenye kijitabu ulichopewa.*
*Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzo wa kila sehemu.*
***Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*© 2018 The Kenya National Examinations Council*

easytvet.com

## SEHEMU A: INSHA (alama 20)

1. Andika insha isiyopungua kurasa mbili wala kuzidi kurasa mbili na nusu ya mojawapo ya vichwa vifuatavyo:

   (a) Simba mwenda pole ndiye mla nyama.

   (b) "Pombe haramu haitaisha nchini milele." Jadili.

   (c) Andika barua ya kutafuta kazi ya uhariri kwa mhariri mkuu wa Gazeti la Taifa Leo.

   (d) Andika ilani itakayochapishwa kwenye gazeti la kila siku kuwaona watu kuhusu kuzuka kwa ugonjwa hatari wa kifua kikuu.

## SEHEMU B: UFAHAMU (alama 30)

2. Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Nimekaa **kutafakari** kwa kipindi kirefu juu ya mabilioni ya pesa ambayo yametengwa na serikali ili kudhamini miradi ya maendeleo ya wanawake. Kina mama au wanawake wengi wanakiri na kusema kwamba fedha hizo zimewawezesha **kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji** kutoka kwa waume zao. Kwani kila mmoja anamheshimu mwenzake kwa sababu ya kipato alicho nacho. Wengi wameweza kuanza biashara ndongondogo ambazo huwaletea angaa kipato kidogo.

Ukweli ni kwamba fedha hizi zimesaidia kuwatoa wanawake wengi katika unyanyasaji, kwani wengi wanaweza kuanzisha kazi za ujasirimali na hata kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo. Kutokana na mafanikio haya, wabunge waliopitisha hoja bungeni za kuanzisha mpango huu wa kuwakwamua wanawake kimaendeleo wanafaa kupongezwa. Mafanikio haya yamewafanya akina mama **kujikimu kimaisha** na hivyo kutowategemea wanaume katika kila jambo. Ukitaka kujua ukweli kuhusu hili, nenda kwenye masoko utaona akina mama jinsi wanavyohangaika na biashara zao. Kwa hivyo ujasirimali huendelezwa na akina mama zaidi na hivyo wanapaswa kuwezeshwa kwa hali na mali.

Akina mama pia wanafaa kupongezwa kwani wameamua kujitosa kukopa fedha kutoka kwenye taasisi mbalimbali za fedha. Fedha hizo kwa kiwango kikubwa zimewainua kutoka katika ufukara uliokithiri hadi katika maisha ya heshima.

Wale ambao hawajajaribu kuchukua mkopo ni muhimu wafanye hivyo ili wajikimu kimaisha. Maisha ya sasa ni magumu, hivyo yanahitaji kusaidiana kwa kila hali na mali. Wanaume kwa wanawake ni vyema wachange bia ili wazumbue **riziki**. Ushirikiano utarahisisha maisha yao. Hata hivyo, sio tu akina mama hao wameondokewa na unyanyasaji waliokuwa wakiupata ndani

easytvet.com

ya nyumba zao, toka kwa akina baba, bali hata masuala ya **mrundiko wa kesi** za kugombea ardhi kwa akina mama, zimepungua. Sababu ni kwamba akina mama wengi wameweza kujitafutia ardhi wenyewe kwa fedha walizonazo.

Ukweli ni kwamba hali imebadilika kinyume na hapo awali, ambapo majumba ya kifahari na mashangingi yalikuwa hifadhi ya wanaume, siku hizi wanawake wanamiliki hayo yote.

**Maswali**

(a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)

(b) Taja dhamira mbili za taarifa hii. (alama 2)

(c) Fafanua jinsi wanaume walikuwa wakirudisha wanawake nyuma. (alama 4)

(d) Sera za serikali zimewasaidia wanawake kivipi? (alama 6)

(e) Kwa nini msimulizi anawapongeza wabunge? (alama 2)

(f) Eleza sababu za baadhi ya wanawake kuishi katika lindi la umaskini kulingana na makala haya. (alama 6)

(g) Mafanikio ya wanawake yanaonekana vipi? Eleza. (alama 2)

(h) Kwa nini wanaume na wanawake wanafaa kusaidiana? (alama 2)

(i) Eleza maana ya msamiati na mafungu ya maneno kama yalivyotumika katika taarifa hii. (alama 5)

(i) kutafakari;
(ii) kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji;
(iii) riziki;
(iv) mrundikiano wa kesi;
(v) kujikimu kimaisha.

easytvet.com

## SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA (alama 30)

*Jibu maswali yote katika sehemu hii.*

3. (a) Taja maana ya maneno yaliyopigiwa msitari katika sentensi hii. (alama 2)

Yule <u>jura</u> anapenda kucheza na <u>chura</u>.

(b) Tambulisha aina za maneno katika sentensi hii. (alama 3)

Huyo kijana mrefu ni mwanafunzi wetu.

(c) Nomino hizi ni za aina gani? (alama 2)

(i) nguo;
(ii) vidole;
(iii) mbwa mwitu;
(iv) baridi;

(d) Ainisha viambishi katika sentensi hii. (alama 3)

Aliyetutembelea.

(e) Kamilisha jedwali hili: (alama 3)

| **Udogo** | **Wastani** | **Ukubwa** |
|---|---|---|
| Kichatu | ______ | ______ |
| ______ | Mkoba | ______ |
| ______ | ______ | Jilango |

(f) Akifisha sentensi hii: (alama 3)

babu babu kofia yako ndio hii mjukuu akamuita babu yake

(g) Tunga sentensi yenye muundo wa: (alama 3)

N + T + U + N + T + E

(h) Toa maana mbili ya sentensi hii: (alama 2)

Chezeni!

easytvet.com

(i) Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa: (alama 2)

"Tukiharakisha tutawapata wezi."
Chifu alisema.

(j) Andika neno jingine lenye maana sawa: (alama 1)

(i) hamaki;
(ii) tamati.

(k) Kanusha sentensi ifuatayo: (alama 2)

Ninamtarajia mwalimu wangu awasili leo.

(l) Kamilisha tashbihi hizi: (alama 2)

(i) Badilika kama;
(ii) Achana kama.

(m) Tegua vitendawili hivi: (alama 2)

(i) Hutembea lakini hakina miguu.

(ii) Mfalme hushuka kwa kelele.

4. **SEHEMU D: MBINU NA VIFAA VYA KUFUNDISHIA** (alama 20)

*Jibu maswali yote katika sehemu hii.*

(a) Wewe kama mwenyekiti wa kikundi cha vijana, umehudhuria maonyesho ya kilimo wilayani mwako. Kwa kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia, eleza vijana kuhusu mbinu mbalimbali za kisasa za kilimo. (alama 10)

(b) Taja na kueleza mbinu mbalimbali utakazotumia kuwafundishia kikundi cha akina mama juu ya faida za muungano wa akina mama. (alama 10)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**